

KUINGIA KWENYE HATARI



David Wilkerson (1931-2011) November 7, 2019

"Kwa hivyo lazima tuzingatie kwa bidii mambo tuliyoyasikia, tusije tukatoweka" (Waebrania 2:1).

Dhambi ya kuwa mbali na Kristo ndiyo mbaya kabisa na hatari katika zambi zote - na hakuna mwamini aliye na kinga. Hata mwamini aliyejitolea zaidi anaweza kuanza kuteleza kwa kuwa muvivu na wazuri juu ya mambo ya Bwana. Mara tu hiyo inapoanza kutokea, inakuwa ngumu zaidi kurudi tena katika ushirika wa karibu na Kristo. Unaweza kuwajua watu fulani ambao hapo zamani walikuwa wakristo wapole, wenye upendo lakini leo wanaonekana kama watu tofauti. Watu wengi wana kazi hawajitambui kuwa wako hatarini.

Historia ya watu wa Mungu imekuwa moja ya kurudi nyuma, kupuuza na kumsahau Mungu. Musa na manabii walionekana kushangazwa na tabia ya watu wa Mungu kwa kumsahau Bwana haraka na kurudi kwenye njia zao za zamani.

Kabla tu ya kufa kwake, Musa aliangalia nyuma historia ya watoto wa Mungu jangwani. Karibu kizazi kizima kilikuwa kikilalamika, kuwarudisha nyuma, watu wasioamini kilikuwa kimeondolewa kwa hukumu ya Mungu, kuliwa katika jangwa lenye moto. Lakini mabaki ya waaminifu – waliyochoka, waliojaribiwa, waliotengwa - walibaki wa kweli kwa Bwana. Musa aliwaambia, "Macho yenu yameona yale Bwana aliotenda huko Baali Peori; kwa maana wote waliomfuata Baal-peori, Bwana Mungu wako, amewaangamiza kutoka kati yako watu wote waliofuata [ibada ya sanamu]. Lakini wewe uliyeshikilia kwa BWANA Mungu wako u hai leo ... Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, Bwana Mungu wetu, alivyo, kwetu, kila tumwitapo?" 4:3-4, 7).

Kwa kweli Musa alikuwa akisema, "Ulikaa ndani ya ukweli wakati wa matendo mkubwa mabaya! Haukuwahi kujitolea katika ibada ya sanamu, kama wale ambao waliangamizwa. Na hakuna mtu aliye na Mungu karibu nao kuliko wewe. "Hao ndio waliingia Nchi ya Ahadi - kwa utimilifu wa Bwana.

Je! Unakumbuka wakati ambao ulihisi kuwa karibu naye zaidi kuliko unavyofanya sasa? Wakati ulisikia uwepo wake kwa urahisi zaidi na kusikia sauti yake wazi zaidi? Inaweza kuwa wakati wa kuchunguza moyo wako ili uhakikishe kama unaendelea kusonga mbere ndani pamoja na Yesu.

[Download PDF](#) [1]

Links

[1] <https://worldchallenge.org/printpdf/31352/>